JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA FEDHA



# BAJETI YA SERIKALI

## YA MWAKA WA FEDHA 2023/24

## KWA LUGHA RAHISI

**Toleo la Mwananchi**



"Bajeti ya Serikali Toleo la Wananchi ni kijitabu kinachoelezea mipango na bajeti ya Serikali kwa muhtasari na lugha rahisi inayoweza kueleweka kwa mwananchi na wadau mbalimbali



# YALIYOMO


1 Utangulizi


2 Vipaumebele vya Bajeti

3 Sera za Bajeti na Uchumi

4 Mapato na Matumizi

5 Mgawanyo wa Bajeti Kisekta

6 Maboresho ya Kodi, Tozo na Ada



# 1. Utangulizi

**Kijitabu hiki kinawasaidia kuielewa na kuifahamu Bajeti ya Serikali kwa mwaka husika na jinsi bajeti inavyoweza kutatua changamoto mbalimbali;**

Bajeti ya Serikali Toleo la Wananchi ni kijitabu kinachotafsiri mipango na bajeti ya Serikali kwa muhtasari na lugha rahisi inayoweza kueleweka kwa mwananchi na wadau mbalimbali. Kijitabu kinasaidia kufahamu mipango na bajeti ya Serikali kwa mwaka husika na jinsi bajeti inavyoweza kutatua changamoto mbalimbali na kuhamasisha dhana ya uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa fedha za umma.

## 1.1 Mchakato wa Bajeti ya Serikali


Bajeti ni nyenzo inayotumiwa na Serikali kutekeleza mipango kwa kugawa rasilimali zilizopo kwa kuzingatia vipaumbele vya Taifa kwa ajili ya ustawi wa jamii. Bajeti ya Serikali huandaliwa kwa kuzingatia: matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977; Sheria ya Bajeti, SURA 439; Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26); na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka husika na huwasilishwa bungeni kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa baada ya kupata ridhaa ya Baraza la Mawaziri. Ratiba ya Maandalizi ya Bajeti ni kama ulivyoainishwa katika Jedwali Na. 1.



# Jedwali Na. 1: Mchakato wa Bajeti ya Serikali

| Mwezi | Shughuli |
|---|---|
| **Agosti - Novemba** | Maandalizi na uidhinishwaji wa Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali |
| **Disemba** | Usambazaji wa Mwongozo wa Mpango na Bajeti ya Serikali |
| **Disemba - Februari** | Maandalizi ya mipango na bajeti za Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali; Sekretarieti za Mikoa; Mamlaka za Serikali za Mitaa; Taasisi na Mashirika ya Umma |
| **Februari - Machi** | Uchambuzi wa mipango na bajeti kisekta |
| **Machi** | Kamati za Kisekta za Bunge kupitia, kuchambua na kuidhinisha mipango na bajeti |
| **Aprili - Juni** | Vikao vya Bunge kujadili na kuidhinisha bajeti ya Serikali |
| **Juni** | Bunge kuidhinisha Sheria ya Fedha na Sheria ya Matumizi ya Serikali |
| **1 Julai - 30 Juni** | Utekelezaji wa mipango na bajeti ya Serikali |

# 2. Vipaumbele vya Bajeti




Katika bajeti ya mwaka 2023/24, Serikali itaendelea kuzingatia maeneo ya vipaumbele vya Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26) ili kuboresha maisha na ustawi wa wananchi ikiwemo kupunguza umaskini pamoja na kuzalisha ajira. Vipaumbele vya bajeti vimejikita katika kuboresha sekta zinazoongeza uzalishaji na kutoa ajira kwa wingi. Sekta hizo ni pamoja na; kilimo, mifugo, uvuvi, nishati, ujenzi, uchukuzi na utalii.

# 3. Uchumi Jumla na Sera za Bajeti

### 3.1 Shabaha za Uchumi Jumla

**Pato la Taifa**

Pato la Taifa linakadiriwa kukua kwa asilimia 5.2 mwaka 2023 kutoka ukuaji wa asilimia 4.7 mwaka 2022

**Mapato ya Kodi**

Mapato ya kodi kufikia asilimia 12.0 ya Pato la Taifa kwa mwaka 2023/24 kutoka asilimia 11.5 ya mwaka 2022/23 na mapato ya ndani kufikia asilimia 14.9 ya Pato la Taifa mwaka 2023/24 kutoka matarajio ya asilimia 14.4 mwaka 2022/23.

**Mfumuko wa Bei**

Mfumuko wa bei unatarajiwa kubaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia 3.0 hadi 7.0 katika kipindi cha muda wa kati.

**Deni la Serikali**

Hadi kufikia Aprili, 2023, deni la Serikali lilikuwa shilingi trilioni 79.1, sawa na ongezeko la asilimia 13.9 ikilinganishwa na shilingi trilioni 69.4 Aprili, 2022. Deni hilo limeongezeka kutokana na kupokelewa kwa mikopo mipya kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, viwanja vya ndege, umeme, kilimo, elimu na afya. Aidha, tathmini ya uhimilivu wa deni la Serikali iliyofanyika mwezi Disemba, 2022 ilionesha kuwa deni la Serikali ni himilivu katika kipindi cha muda wa kati na mrefu.

## 3.2 Mikakati ya Kuongeza Mapato ya Serikali


i. Kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ikiwemo kuendelea kufanya marekebisho ya sheria mbalimbali ili kuongeza ushiriki wa sekta binafsi;

ii. Kuongeza wigo wa mapato kwa kusajili biashara na walipakodi wapya pamoja na kuendelea na jitihada mbalimbali za kuziba mianya ya ukwepaji kodi na kutoa elimu kwa umma kuhusu ulipaji kodi wa hiari;

iii. Kuimarisha na kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali;

iv. Kuendelea kusimamia Wizara na Taasisi za Serikali kutumia Mfumo wa Serikali wa Kieletroniki wa Ukusanyaji wa Mapato (GePG) na kuhakikisha malipo yote ya Serikali yanafanyika kwa kutumia namba ya kumbukumbu ya malipo (Control number);

v. Kusimamia matumizi sahihi ya EFD ili kudhibiti upotevu wa mapato na kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa kodi;




vi. Kudhibiti misamaha ya kodi ili isizidi asilimia moja (1) ya Pato la Taifa kwa: kufanya tathmini ya mfumo wa kisheria unaotumika

kutoa na kusimamia motisha za kikodi ili kubaini ufanisi katika kufikia malengo tarajiwa; na kuboresha pamoja na kuhamasisha uwekezaji kwa kutumia vivutio visivyo vya kikodi kama vile ardhi, miundombinu ya maji, barabara na nishati;




vii. Kufanya tafiti na tathmini zinazolenga kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali na kuibua vyanzo vipya vya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi;


viii. Kuendelea kuimarisha mifumo na usimamizi wa Mashirika, Taasisi za umma na Wakala za Serikali ili kuongeza ufanisi na kuhakikisha gawio na michango stahiki inawasilishwa Mfuko Mkuu wa Serikali kwa wakati;

ix. Kuendelea kutoa elimu kwa umma ili kuhamasisha uwekezaji kwenye soko la ndani la dhamana za Serikali;

x. Kuimarisha ushirikiano na Washirika wa Maendeleo ikiwa ni pamoja na kutekeleza makubaliano ya kimkataba ili kuwezesha upatikanaji wa misaada na mikopo kama ilivyopangwa; na


xi. Kutumia fursa iliyopatikana kutokana na zoezi la credit rating ili kuongeza mitaji ya uwekezaji kutoka kwenye soko la fedha la kimataifa kwa ajili ya kuwekeza kwenye miradi mikubwa ya maendeleo.

## 3.3 Mikakati ya Usimamizi wa Matumizi ya Serikali




i. Kuendelea kusimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia sheria na miongozo iliyopo;
ii. Kuendelea kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika utekelezaji wa shughuli za Serikali ili kubana matumizi ikiwa ni pamoja na kuendesha vikao kwa njia ya mtandao na kupunguza matumizi ya karatasi;
iii. Kuimarisha usimamizi wa mashirika, wakala na taasisi za Serikali ili yajiendeshe kwa ufanisi na kuipunguzia mzigo Serikali;
iv. Kuimarisha usimamizi wa miradi kwa kufanya ukaguzi wa ufanisi kwa wakati ili kuokoa gharama za ziada zinazoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa miradi; na
v. Kufanya mapitio ya Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 ili kufanya mfumo wa ununuzi wa umma kuwa wa kimkakati pamoja na kuziba mianya ya ubadhirifu kwa lengo la kupata thamani ya fedha katika matumizi ya Serikali.







# 4. Mapato na Matumizi

Katika mwaka 2023/24, Serikali imepanga kukusanya na kutumia jumla ya shilingi trilioni 44.39.

## Mchanganuo wa mapato ya Serikali kwa mwaka 2023/24



## Mchanganuo wa matumizi ya Serikali kwa mwaka 2023/24




### 4.1 Mgawanyo wa Matumizi kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa

Baadhi ya maeneo yaliyopewa kipaumbele katika matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ni:

i. Shilingi bilioni 399.6 kwa ajili ya Elimu Bila Ada Kwa Shule Za Msingi Na Sekondari;

ii. Shilingi bilioni 243.6 kwa ajili ya usimamizi wa mitihani ya Kitaifa;

iii. Shilingi bilioni 107.3 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa, mabwalo, mabweni, matundu ya vyoo na ukarabati wa shule kongwe za msingi na sekondari;


iv. Shilingi bilioni 79.3 kwa ajili ya ujenzi majengo ya utawala, nyumba za Wakurugenzi na Wakuu wa Idara;


v. Shilingi bilioni 86.4 kwa ajili ya ukamilishaji wa vituo vya afya, zahanati, hospitali za wilaya ukarabati na hospitali kongwe za halmashauri; na

vi. Shilingi bilioni 36.7 kwa ajili ya kulipa posho za madiwani na Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo.


"
Shilingi bilioni 86.4 kwa ajili ya ukamilishaji wa vituo vya afya, zahanati, hospitali za wilaya ukarabati na hospitali kongwe za halmashauri

# 5. Mgawanyo wa Bajeti Kisekta




## 5.1 Sekta ya Elimu

Sekta hii imetengewa shilingi trilioni 5.9. Maeneo ya vipaumbele ni kama ifuatavyo:

i. Shilingi trilioni 4.5 kwa ajili ya kugharamia elimu ya awali, elimu ya msingi, elimu ya sekondari, vyuo vya ualimu, ukaguzi wa shule, elimu ya watu wazima na elimu isiyo rasmi;
ii. Shilingi trilioni 1.2 kwa ajili ya elimu ya juu ikijumuisha shilingi bilioni 738.7 za mikopo ya elimu ya juu;
iii. Shilingi bilioni 144.4 kwa ajili ya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi ikijumuisha bilioni 18.0 za mikopo ya elimu ya kati;
iv. Shilingi bilioni 116.9 kwa ajili ya matumizi ya huduma za utawala; na
v. Shilingi bilioni 61.4 kwa ajili ya sayansi na teknolojia.

## 5.2 Sekta ya Afya

Sekta hii imetengewa jumla ya shilingi trilioni 2.5. Baadhi ya maeneo ya kipaumbele ni kama ifuatavyo:

i. Shilingi bilioni 978.4 kwa ajili ya kuboresha huduma za tiba na miundombinu katika hospitali za rufaa ngazi ya kanda na taifa;

ii. Shilingi bilioni 821.9 kwa ajili ya kuboresha huduma na miundombinu ya afya katika hospitali za wilaya;

iii. Shilingi bilioni 307.7 kwa ajili ya huduma za kinga ikiwemo ununuzi na usambazaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba, vitendanishi na chanjo;

iv. Shilingi bilioni 247.9 kwa ajili ya kuboresha huduma na miundombinu ya afya katika zahanati na vituo vya afya; na

v. Shilingi bilioni 107.6 kwa ajili ya kugharamia shughuli za utawala na rasilimali watu katika utoaji wa huduma za afya.

## 5.3 Sekta ya Ulinzi, Usalama na Utii wa Sheria

Serikali imetenga shilingi trilioni 4.7 sawa kwa ajili ya kuimarisha ulinzi wa nchi; kudumisha amani na usalama wa raia na mali zao; na kuimarisha utawala wa Sheria.

## 5.4 Sekta ya Huduma za Utawala na Deni la Serikali

Sekta hii imetengewa shilingi trilioni 11.8 kugharamia shughuli mbalimbali kama ifuatavyo:

i. Shilingi trilioni 4.2 kwa ajili ya kugharamia malipo ya riba;

ii. Shilingi trilioni 4.2 kwa ajili ya shughuli za utawala;

iii. Shilingi trilioni 3.2 kwa ajili ya shughuli za fedha na uchumi ikijumuisha shilingi bilioni 200 za maandalizi ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa; na

iv. Shilingi bilioni 247.7 kwa ajili ya shughuli za mambo ya nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.


## 5.5 Sekta ya Hifadhi ya Jamii

Serikali imetenga shilingi trilioni 2.3 kwa ajili ya Sekta ya Hifadhi ya Jamii. Baadhi ya shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na: kuwezesha makundi maalum kiuchumi kama vile wamachinga; kuboresha miundombinu katika vyuo vya maendeleo ya jamii; kuwekeza katika afya na maendeleo ya vijana balehe; kuboresha huduma kwa wazee hususan huduma za afya kwa kutoa bima ya matibabu bure (ICHF); na kugharamia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Mfuko wa Bima ya Afya.




## 5.6 Sekta ya Maendeleo ya Uchumi

Sekta hii imetengewa jumla ya shilingi trilioni 9.4 ili kutekeleza vipaumbele mbalimbali ambavyo vitakavyo chochea ukuaji wa uchumi wa Taifa.




### 5.6.1 Sekta ya Kilimo

Sekta hii inayojumuisha kilimo, umwagiliaji, mifugo na uvuvi imetengewa jumla ya shilingi trilioni 1.47 kwa ajili ya kutekeleza mipango na vipaumbele mbalimbali kama ifuatavyo:

i. Shilingi bilioni 262.3 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa mabwawa na skimu za um wagiliaji ili kuongeza eneo la umwagiliaji kwa hekta 256,185.46;

ii. Shilingi bilioni 130.0 kwa ajili ya ruzuku ya mbolea;

iii. Shilingi bilioni 83.8 ni za utafiti na uzalishaji mbegu bora;



iv. Shilingi bilioni 61.9 kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa skimu na mabwawa ya umwagiliaji;
v. Shilingi bilioni 50.7 kwa ajili ya pembejeo za korosho;
vi. Shilingi bilioni 50.0 za ujenzi wa bandari ya uvuvi;
vii. Shilingi bilioni 49.5 kwa ajili ya ufugaji wa samaki, uwekezaji wa kibiashara katika uvuvi na kuanzisha mashamba darasa ya samaki;
viii. Shilingi bilioni 45.5 ni kwa ajili ya maendeleo ya malisho ya mifugo, kuongeza uzalishaji wa mifugo na masoko, utafiti, mafunzo pamoja na huduma za ugani;
ix. Shilingi bilioni 40.0 ni mtaji kwa Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC) ili kuwekeza na ku punguza uagizaji wa mbolea nje ya nchi;
x. Shilingi bilioni 38.7 kwa ajili ya huduma za ugani na miundombinu ya kuhifadhia mazao;
xi. Shilingi bilioni 14.2 kwa ajili ya kuendeleza mashamba makubwa ya pamoja (BBT); na
xii. Shilingi bilioni 2.2 kwa ajili ya uimarishaji wa huduma za ushirika kwa kusajili vyama vya ushirika.

## 5.6.2 Sekta ya Madini

Sekta ya Madini imetengewa shilingi bilioni 89.3 ili kutekeleza baadhi ya vipaumbele ikijumuisha ununuzi mitambo miwili (2) ya uzalishaji wa makaa ya mawe ya kupikia, ununuzi wa mtambo mmoja wa kuchakata madini ya chokaa, tafiti za Madini, ununuzi wa vifaa vya maabara za jiosayansi, huduma za ugani, uanzishwaji wa minada ya madini ya vito na kujenga uwezo wa usimamizi endelevu wa Sekta ya Madini; na kujenga na kupanua miundombinu ya Kituo cha Jeomolojia.



### 5.6.3 Sekta ya Nishati

Sekta ya Nishati imetengewa shilingi trilioni 3.0 ili kutekeleza vipaumbele mbalimbali ikiwemo:

i. Shilingi trilioni 1.9 kwa ajili ya miradi ya kuzalisha umeme ikijumuisha shilingi trilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa Bwawa la Julius Nyerere Megawati 2115;
ii. Shilingi bilioni 473.4 kwa ajili ya ukarabati na uboreshaji wa Gridi ya Taifa ;
iii. Shilingi bilioni 434.9 kwa ajili ya usambazaji umeme vijijini;
iv. Shilingi bilioni 186.2 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kusafirisha, kusambaza na kupooza umeme; na
v. Shilingi bilioni 174.0 kwa ajili ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika vitalu vya kimkakati na ujenzi wa miundombinu ya gesi asilia na mafuta.



## 5.6.4 Sekta ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Katika bajeti ya mwaka 2023/24, Sekta ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano imetengewa jumla ya shilingi trilioni 3.8 ili kutekeleza vipaumbele mbalimbali ikiwemo:

### Ujenzi

i. Shilingi trilioni 1.2 kwa ajili ya ujenzi wa barabara na madaraja;
ii. Shilingi trilioni 1.3 kwa ajili ya ukarabati wa mtandao wa barabara, ikijumuisha shilingi bilioni 599 za barabara kuu na mikoa na shilingi bilioni 710.3 za barabara za mijini na vijijini;
iii. Shilingi bilioni 96.8 kwa ajili ya miradi ya ujenzi wa miundombinu ya viwanja vya ndege;
iv. Shilingi bilioni 45.0 kwa ajili ya ujenzi wa Barabara ya Mzunguko wa Nje katika Jiji Dodoma;
v. Shilingi bilioni 38.8 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo ya Serikali na Nyumba za Viongozi; na
vi. Shilingi bilioni 14.2 kwa ajili ya ujenzi na ukaraba ti wa vivuko.




### Uchukuzi

i. Shilingi trilioni 1.1 kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR);
ii. Shilingi bilioni 294.8 kwa ajili ya kuboresha usafiri wa njia ya reli kupitia Mfuko wa Reli;
iii. Shilingi bilioni 271.0 kwa ajili ya ununuzi na ukarabati wa ndege;
iv. Shilingi bilioni 90.2 kwa ajili ya kusimamia ubora wa huduma za usafiri wa anga kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Anga;
v. Shilingi bilioni 46.3 kwa ajili ya kugharamia uendeshaji na uwekaji miundombinu ya vi wanja vya ndege nchini; na
vi. Shilingi bilioni 13.0 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na miundombinu ya rada na hali ya hewa nchini.

### Mawasiliano

i. Shilingi bilioni 80.0 kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano; na
ii. Shilingi bilioni 24.0 kwa ajili ya mradi wa Mfumo wa Anwani za Makazi nchini.

### 5.6.5 Sekta ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara

Serikali katika jitihada za kujenga na kuimarisha misingi thabiti ya uchumi wa kuvutia wawekezaji na ujenzi wa viwanda kama ilivyobainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, imetenga jumla ya shilingi bilioni 352.9 kwa ajili ya kutekeleza vipaumbele mbalimbali ikiwemo:

i. Miradi ya kielelezo ya Magadi Soda Engaruka, Makaa ya Mawe – Mchuchuma na Chuma – Liganga;
ii. Kuimarisha Uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma;
iii. Uwekezaji katika maeneo maalum ya kiuchumi (SEZ) na kongani za viwanda;
iv. Kuboresha mazingira ya biashara;
v. Kukuza uwezeshaji wananchi kiuchumi; na
vi. Kuimarisha huduma za biashara na masoko.



## 5.6.6 Sekta ya Maliasili, Utalii na Mazingira

### Maliasili, Utalii

Katika mwaka 2023/24, ili kuhakikisha Serikali inaendelea kuhifadhi, kutunza, kusimamia ma-liasili na kuendeleza sekta ya utalii nchini, shilingi bilioni 649.1 zimetengwa katika kwa ajili ya kutekeleza vipaumbele muhimu ikiwemo:-

i. Shilingi bilioni 108.9 kwa ajili ya kulinda na kuhifadhi rasilimali za wanyamapori na
ii. kuimarisha ardhioevu;
iii. Shilingi bilioni 154.8 kwa ajili ya kuendeleza na kutunza misitu pamoja na ufugaji wa nyuki; (hii ipo kwenye Sekta ya Kilimo)
iv. Shilingi 167.2 kwa ajili ya kuendeleza na kuimaisha miundombinu ya utalii pamoja na kutangaza na utalii endelevu kupitia kwa Programu maalum ya kutangaza nchi ijulikanayo kama Tanzania – *the Royal Tour*



## Mazingira

Katika mwaka 2023/24, Serikali inaenedelea kutekeleza uhifadhi na usimamizi endelevu wa Mazingira nchini, ambapo shilingi bilioni 39.4 zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza vipaumbele muhimu ikiwemo:-


i. Shilingi bilioni 2.6 kwa ajili ya kujenga uwezo wa taasisi kusimamia Sheria ya mazingira ikiwa ni pamoja na kuandaa kanuni tano (5), miongozo mitano ya usimamizi wa mazingira, kanzi data ya tathmini ya mazingira pamoja na kuanzisha Jukwaa la kitaifa la usimamizi wa mazingira;

ii. Shilingi bilioni 1.0 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa kingo katika fukwe za Mikindani na Sipwese; na

iii. Shilingi milioni 850.8 kwa ajili ya mradi wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika jamii zinazozunguka misitu ya miombo Tanzania Bara na Zanzibar.

iv. Shilingi bilioni 4.0 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji, majosho 14, visima virefu sita (6) malambo matatu (3) na kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa vijiji 38 na urejeshaji wa misitu na mazingira;

v. Shilingi bilioni 3.5 kwa ajili ya kuendelea na uchimbaji visima virefu viwili (2), uchimbaji wa malambo matatu (3), ujenzi wa kiwanda kidogo cha bidhaa za ngozi; kukamilisha ujenzi wa mabirika manne ya kunyweshea mifugo; na utengenezaji wa majiko banifu na uzalishaji wa gesi inayotokana na samadi;




### 5.6.7 Sekta ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Kukuza Ujuzi

Katika mwaka 2023/24 shilingi bilioni 20.3 zimetengwa kwa ajili ya Sekta ndogo ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Kukuza Ujuzi kama ifuatavyo:

i. Shilingi bilioni 9.0 kuwezesha Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini kwa ajili ya kutoa mafunzo ya ujuzi mbalimbali kwa vijana kupitia taasisi za mafunzo;

ii. Shilingi bilioni 8.9 kuwezesha shughuli za kazi na ajira ikijumuisha kuimarisha Ofisi za kazi mikoa na kuwezesha uratibu wa masuala ya ukuzaji wa fursa za ajira;

iii. Shilingi bilioni 1.3 kuwezesha Programu ya kukuza Kazi za Staha; na

iv. Shilingi bilioni 1.0 kuwezesha Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa vikundi vya vijana.

### 5.7 Sekta ya Maji, Makazi na Maendeleo ya Jamii

Sekta hii imetengewa jumla ya shilingi trilioni 1.3 ilikutekeleza vipaumbele mbalimbali vitakavyowezesha: kuongezeka kwa upatikanaji wa huduma wa maji safi na salama na toshelevu nchini; kupanga, kupima na kumilikisha ardhi; kuboresha utoaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii; pamoja na kukuza, kuendeleza sanaa, michezo na utamaduni.

### 5.7.1 Sekta ya Maji

Kwa mwaka 2023/24, Sekta ndogo ya Maji imetengewa shilingi bilioni 766.2 ili kutekeleza baadhi ya vipaumbele kama ifuatavyo:

i. Shilingi bilioni 317.3 kwa ajili ya kusambaza maji vijijini na usafi wa mazingira;

ii. Shilingi bilioni 213.5 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya kusambaza maji mjini;

iii. Shilingi bilioni 61.9 kwa ajili ya ujenzi wamabwawa ya Kidunda na Kipera;

iv. Shilingi bilioni 41.5 kwa ajili ya kuendeleza na kutunza vyanzo vya maji nchini; na

v. Shilingi bilioni 35.4 kwa ajili ya kuboresha huduma za usambazaji wa maji katika Jiji la Dar es Salaam na maeneo ya jirani.

### 5.7.2 Sekta ya Ardhi, Nyumba na Makazi

Sekta ndogo ya Ardhi, Nyumba na Makazi imetengewa shilingi bilioni 175.3 kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali za kipaumbele. Miongoni mwa vipaumbele hivyo ni:




i. Shilingi bilioni 1.06 kujenga na kukarabati majengo;

ii. Shilingi bilioni 68.71 kuboreshaji milki zaardhi;

iii. Shilingi bilioni 2.45 kuimarisha mipaka yakimataifa;

iv. Shilingi bilioni 4.53 Kupanga, Kupima na-Kumilikisha (KKK) ardhi; na

v. Shilingi bilioni 5.38 kuimarisha miudombinu ya upimaji na ramani.

### 5.7.3 Sekta ya Maendeleo ya Jamii

Katika mwaka 2023/24, ili kuhakikisha Serikali inaendelea kuboresha utoaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii, shilingi bilioni 369.8 zimetengwa katika sekta hii kutekeleza vipaumbele muhimu vifuatavyo :-

i. Shilingi bilioni 309.6 kwa ajili ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo na ustawi wa jamii;

ii. Shilingi bilioni 18.5 kwa ajili ya kutambua na kuratibu Makundi Maalum wakiwemo wafanyabiashara ndogondogo ili kuboresha mazingira ya biashara zao kwa kupewa mikopo yanye masharti nafuu;

iii. Shilingi bilioni 4.9 kwa ajili ya kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake kiuchumi;

iv. Shilingi bilioni 3.6 kwa ajili ya kuratibu utoaji wa huduma za msingi kwa watu



wenye mahitaji maalum ikiwemo huduma za msaada wa kisaikolojia kwa manusura wa majanga mbalimbali na makundi mengine yenye uhitaji katika jamii;

v. Shilingi bilioni 3.1 kwa ajili ya Ujenzi na uboreshaji wa Miundombinu katika Taasisi na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii nchini;

vi. Shilingi bilioni 2.6 kwa ajili ya uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;

vii. Shilingi bilioni 1.8 kwa ajili ya kuratibu na kuwezesha upatikanaji wa haki za watoto na huduma za ustawi wa jamii kwa wazee; na

viii. Shilingi bilioni 1.3 kwa ajili ya kuratibu utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA).

### 5.7.4 Utamaduni, Sanaa na Michezo

Shilingi bilioni 35.4 zimetengwa kwa ajili ya kukuza, kuendeleza sanaa, michezo na utamaduni. Baadhi ya maeneo ya vipaumbele ni pamoja na: kukarabati, kuboresha, kujenga na kutunza miundombinu ya utamaduni, sanaa na michezo; kuziwezesha ushiriki wa Timu za Taifa katika mashindano mbalimbali ya Kimataifa; kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika kukuza na kuendeleza shughuli za utamaduni, sanaa na michezo; na kuratibu matamasha na matukio makubwa ya utamaduni, sanaa na michezo.

# 6.0 Maboresho ya Kodi, Tozo na Ada

Serikali imeendelea kufanya marekebisho ya sheria za kodi, tozo na ada mbalimbali. Baadhi ya marekebisho hayo ni kama ifuatavyo:

i. Kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye uuzaji na ukodishaji wa ndege, injini za ndege na vifaa vyake vinavyouzwa nchini;
ii. Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha Shilingi 20 kwa kila kilo moja ya Saruji inayotoka nje ya nchi na inayozalishwa ndani ya nchi;
iii. Kuongeza kima cha usajili kwenye Kodi ya Ongezeko la Thamani kinachotakiwa kwa mfanyabiashara kusajiliwa kutoka shilingi milioni 100 hadi shilingi milioni 200;
iv. Kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kiwango cha asilimia 0 kwenye mbolea inayozalishwa ndani ya nchi kwa kipindi cha mwaka 1;
v. Kubadilisha Kodi ya Ongezeko la Mtaji (Capital Gain Tax) kutoka asilimia 10 kwenye faida kuwa Kodi ya Mapato ya asilimia 3 ya thamani ya mauzo au thamani ya ardhi iliyothaminishwa, (thamani yoyote kubwa kati ya hizo) kwa walipakodi wasiotunza kumbukumbu za manunuzi au uendelezaji wa mali husika;
vi. Kutoza Kodi ya Mapato kwa kiwango cha asilimia 2 kwenye malipo ya wachimbaji wadogo wa madini;
vii. Kutoza Kodi ya Mapato kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye malipo yatokanayo na uuzaji wa hewa ukaa;
viii. Kufanya marekebisho ya viwango maalum vya ushuru specific duty rates kwa kiwango cha asilimia 10 ya bei kwenye bidhaa zisizo za petrol, na asilimia 20 ya bei kwenye bidhaa za bia na tumbaku;
ix. Kusamehe ushuru wa bidhaa unaotozwa kwa mujibu wa uwezo wa injini (engine capacity) kwenye magari yanayotumia nishati ya umeme pekee pamoja na magari yanayotumia nishati ya gesi asilia pekee.

x. kushusha kiwango cha sasa cha adhabu inayotozwa kwa makosa ya kutotoa risiti au kutotumia mashine za kielektroniki (EFD) kinachoanzia shilingi 4,500,000 hadi shilingi 3,000,000 kwenda asilimia 20 ya thamani ya kodi iliyokwepwa au shilingi 3,000,000 kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa; na


xi. Kushusha kiwango cha adhabu inayotozwa kwa makosa ya kutodai risiti au kutotoa taarifa ya makosa ya kutotoa risiti cha shilingi 30,000 hadi shilingi 1,500,000 kwenda asilimia 20 ya thamani ya kodi iliyokwepwa au shilingi 30,000 kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa;

xii. Kupunguza kiwango cha tozo ya mabango yasiyowaka ya matangazo (non-illuminated) kutoka shilingi kwenye 10,000 hadi shilingi 7,000 na kuhamisha jukumu la kukusanya ushuru wa mabango kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania kwenda kwa Ofisi ya Rais – Tawala za Miko ana Serikali za Mitaa (TAMISEMI);

xiii. Kuongeza ushuru wa barabara na mafuta kwa kiasi cha shilingi 100 kwa kila lita ya mafuta ya petroli na dizeli;

xiv. Kupunguza kiwango cha tozo ya ufundi stadi kutoka asilimia 4 hadi asilimia 3.5;

xv. Kutoa hati ya ukaazi (Residence Permit Class B) kwa mwekezaji yeyote asiye mkaazi hapa nchini na atakayewekeza kununua nyumba kwa mtaji usiopungua dola za Kimarekani 150,000;



# Jedwali Na. 2: Muhtasari wa Bajeti kwa Kila Sekta

| SEKTA | Bajeti 2023/24 Bilioni | Asilimia (%) |
|---|---|---|
| **Utawala na Deni la Serikali** | **11,788.3** | **31.03** |
| erikali (Ulipaji wa Riba) | 4,163.80 | 10.9 |
| | 4,185.70 | 11 |
| a Nje na Ushirikiano wa Kimataifa | 247.7 | 0.7 |
| zi wa mapato na Matumizi | 3,191.2 | 8.5 |
| **vala wa Sheria na Usalama** | **4,688.30** | **12.3** |
| | 2,987.30 | 7.8 |
| na | 413.3 | 1.1 |
| wa Umma | 1,287.70 | 3.4 |
| **a Uchumi** | **9,470.1** | **24.8** |
| | 1,465.20 | 3.8 |
| | 3,048.60 | 8 |
| | 110.4 | 0.3 |
| endeleo ya Vijana na Kukuza Ujuzi | 20.3 | 0.1 |
| | 89.3 | 0.2 |
| Utalii na Mazingira | 649.1 | 1.7 |
| | 242.5 | 0.5 |
| chukuzi na Mawasiliano | 3,844.60 | 10.1 |
| | **5,979.60** | **15.7** |
| ingi | 4,485.10 | 11.8 |
| za Utawala | 122.9 | 0.3 |
| Juu | 1,165.90 | 3.1 |
| Teknolojia na Ubunifu | 61.4 | 0.2 |
| Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi | 144.4 | 0.4 |
| | **2,463.7** | **6.47** |
| za Tiba | 978.1 | 2.6 |
| | 92.8 | 0.2 |
| za Wilaya | 821.9 | 2.2 |
| za Utawala | 107.6 | 0.3 |
| a Afya | 155.2 | 0.4 |
| za Kinga | 308.1 | 0.8 |
| za Rufaa za Mikoa | - | - |
| **i na Maendeleo ya Jamii** | **1,346.70** | **3.54** |
| o ya Jamii | 369.8 | 1 |
| Michezo na Utamaduni | 35.4 | 0.1 |
| yumba na Makazi ya Watu | 175.3 | 0.5 |
| | 766.2 | 2 |
| **amii** | **2,345.50** | **6.16** |
| Watoto na Watu wenye Ulemavu | 52.3 | 0.1 |
| a Bima wa Afya | 445.9 | 1.2 |
| a Hifadhi ya Jamii | 1,847.30 | 4.9 |
| **kta** | **38,082.10** | **100.00** |
| **kali (Ulipaji wa Mtaji)** | **6,306.00** | |
| | **44,388.10** | |



## NYARAKA REJEA ZA BAJETI

Ifuatayo in orodha ya nyaraka zinazochapishwa na Serikali na kutumika kama chanzo cha taarifa za kuandaa bajeti:

1. Dira ya Maendeleo ya Tanzania, 2025
2. Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano;
3. Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi ya Mkuu wa Mwaka 2020;
4. Mfumo wa Sera za Uchumi Jumla: Unatoa taarifa juu ya sera za bajeti na maboresho;
5. Randama za Mipango ya Muda wa Kati na Mfumo wa Matumizi wa Muda wa Kati ya mwaka 2023/24;
6. Mwongozo wa Mipango na Bajeti 2023/24;
7. Hotuba za Bajeti za Wizara za Mwaka wa Fedha 2023/24;
8. Hotuba ya Bajeti ya Serikali ya Mwaka wa fedha 2023/24;
9. Sheria ya Fedha ya Mwaka 2020;
10. Sheria ya Matumizi ya mwaka 2020;
11. Sheria ya Bajeti ya 2015, Sura 439;
12. Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/24 (Juzuu Na. I, II, III na IV);

Ili kupata baadhi ya nyaraka hizi na matoleo yaliyotangulia ya vitabu vya Bajeti ya Serikali Toleo la Mwanachi, unaweza kutembelea mitandao ya:

» Wizara ya Fedha na Mipango (www.mof.go.tz )

» Policy Forum (www.policyforum.or.tz)

Kwa maelezo zaidi kuhusu Bajeti ya Serikali unaweza kupata taarifa zaidi kuhusu mchakato wa uandaaji wa bajeti kutoka katika vyanzo vifuatavyo:

» Nyaraka zenye taarifa za Bajeti ya Serikali (angalia orodha ya nyaraka za rejea) na hasa, nakala ngumu ya vitabu vya Bajeti ya Serikali ambavyo vinapatikana Wizara ya Fedha na Mipango S.L.P 2802, Dodoma.

» Nakala laini za vitabu vya Bajeti ya Serikali zinaatikana kwenye tovuti ya Wizara ya Fedha na Mipango (www.mof.go.tz )

Kumbuka kwamba ni haki yako kujua bajeti hii na taarifa nyingine zinazohusiana na Bajeti ya Serikali. Ongea na Viongozi wako kuhusu taarifa hizi na washirikishe watu wengine katika jamii unayoishi nayo.

Kwa maoni yako jaza ukurasa huu na kutuma Wizara ya Fedha na Mipango

Toa maoni yako kuhusu Bajeti ya Serikali ya mwaka 2023/24

--------------------------------------------------------------------------------

--------------------------------------------------------------------------------

--------------------------------------------------------------------------------

Je, unahitaji ufafanuzi zaidi ya uliotolewa katika kitabu hiki?

☐ NDIYO ☐ HAPANA

Kama jibu ni NDIYO Je, unahitaji ufafanuzi katika eneo gani?

--------------------------------------------------------------------------------

--------------------------------------------------------------------------------

--------------------------------------------------------------------------------

Je, ni kwa kiasi gani kitabu hiki kimekusaidia?

☐ Kiasi kikubwa ☐ Wastani ☐ Hakikunisaidia

Je, ni kwa kiasi gani kitabu hiki kilikuwa rahisi kusoma na kueleweka?

☐ Rahisi ☐ Wastani ☐ Ngumu

Tuma maoni yako katika anuani ifuatayo

Katibu Mkuu,
Wizara ya Fedha na Mipango,
Idara ya Usimamizi wa Bajeti ya Serikali,
Mtaa wa Hazina,
Mji wa Serikali – Mtumba,
40468 Dodoma,
Sanduku la Barua 2802,
DODOMA-TANZANIA
Au tuma kwa njia ya barua pepe kwa:
ps@mof.go.tz



**Address**

Mji wa Serikali - Mtumba,
Mtaa wa Hazina
S. L. P 2802,
40468 Dodoma.

**Contact**

info@hazina.go.tz,
+255 26 2160000
www.mof.go.tz



# BAJETI YA SERIKALI
## YA MWAKA WA FEDHA 2023/24
## KWA LUGHA RAHISI